

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS

### SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na EA.7/96/01/L/142

11 Juni, 2021

### TANGAZO LA MAOMBI YA KUHAMIA KATIKA SHIRIKA LA MAWASILIANO TANZANIA (TTCL)

Kwa niaba ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anakaribisha maombi ya kuhamia katika Shirika la Mawasiliano Tanzania kwa watumishi wa Umma ili kujaza nafasi **tisa (9)** kama zilizyoainishwa katika tangazo hili.

#### 1.0.1 MKAGUZI WA NDANI MWANDAMIZI – (NAFASI 1)

#### 1.0.2. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. **Awe ni mwajiriwa katika Utumishi wa umma,**
- ii. Awe na Shahada ya kwanza katika Uhasibu, Fedha, Usimamizi wa biashara/ Biashara inayojumuisha Uhasibu au Fedha au sifa sawia kwa Taasisi inayotambuliwa pamoja na CPA (T), ACCA, ACA, CIA au sifa sawia ya kitaalam inayotambuliwa na NBAA.
- iii. Uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba (7) katika fani inayohusiana

#### 1.0.3. MSHAHARA

Ngazi ya mshahara: TTCS 7

## 2.0. MHASIBU MWANDAMIZI - (NAFASI 8)

### 2.0.1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. **Awe ni mwajiriwa katika Utumishi wa umma,**
- ii. Awe na Shahada ya kwanza katika Uhasibu, Fedha, Usimamizi wa biashara/ Biashara inayojumuisha Uhasibu au Fedha au sifa sawia kwa Taasisi inayotambuliwa pamoja na CPA (T), ACCA, ACA, CIA au sifa sawia ya kitaalam inayotambuliwa na NBAA.
- iii. Uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba (7) katika fani inayohusiana

### 2.0.2. MSHAHARA

Ngazi ya mshahara: TTCS 7

### MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji wapitishie barua zao za maombi ya kuhamia kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, taaluma, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye tangazo vilivyothibitishwa (certified as true copies)
- vi. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**

viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

ix. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 23 Juni, 2021.**

**Muhimu, kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kuhamia iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Barua hiyo ielekezwe kwa;**

**KATIBU  
OFISI YA RAIS  
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA  
S.L.P. 2320 DODOMA.**

i. *Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;*

*<http://portal.ajira.go.tz/>*

*(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa '**Recruitment Portal**')*

ii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

**KATIBU  
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**